BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTARATIBU WA KUBAINISHA NA KUWATAMBUA WANAFUNZI WAHITAJI (MEANS TESTING)

1.0 UTANGULIZI.

Uchangiaji katika huduma mbalimbali za jamii ulianza kutekelezwa nchini tangu mwaka 1992. Katika elimu ya juu, sera hiyo ilianza kutekelezwa kwa awamu kama ifuatavyo:-

(i) Awamu ya kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 1992/1993. Katika awamu hii, wanafunzi walitakiwa kuchangia gharama za usafiri wa kwenda na kurudi vyuoni, michango ya serikali za wanafunzi, vitambulisho, ada ya maombi, ada ya usajili, matibabu na fedha za tahadhari.

(ii) Awamu ya Pili ilianza kutekelezwa mwaka 1994/1995. Katika awamu hii, pamoja na maeneo ya uchangiaji katika awamu ya kwanza, wanafunzi walitakiwa kuchangia gharama za chakula na malazi ambazo zilitolewa kama mikopo kupitia iliyokuwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya juu.

(iii) Awamu ya tatu ilianza kutekelezwa mwaka 2005/2006, kufuatia kuundwa kwa Bodi ya Mikopo ambayo ilipewa jukumu la kutoa mikopo kwa wanafunzi badala ya mikopo hiyo kutolewa moja kwa moja na Serikali. Katika awamu hii, pamoja na maeneo ya uchangiaji katika awamu ya kwanza na ya pili, wanafunzi walitakiwa kuchangia pia katika ada ya mafunzo, vitabu na viandikwa, mahitaji maalumu ya vitivo na gharama za mafunzo kwa vitendo.

Madhumuni makuu ya sera ya uchangiaji wa gharama za elimu ya juu hususan kwa kutumia utaratibu wa mikopo ni:

- Kupanua udahili katika vyuo vya elimu ya Juu ili wanafunzi wengi zaidi waweze kupata elimu ya juu.

- Kuwawezesha wanafunzi ambao hawana uwezo wa kiuchumi kugharamia elimu ya juu kwa njia ya mikopo.

- Kuhuisha matumizi ya fedha chache zilizopo ili kuimarisha na kuboresha miundo mbinu ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya elimu ya juu.

- Kuwa na njia ya uhakika zaidi ya kugharamia elimu ya juu (Revolving fund)

2.0 JUKUMU LA KUWEKA UTARATIBU WA KUWATAMBUA WANAFUNZI WAHITAJI WA MIKOPO (MEANS TESTING)

Kutokana na uchanga katika jukumu la utoaji wa mikopo ya wanafunzi na kutokana na uchache wa wafanyakazi na vitendea kazi pamoja na kutokuwepo mfumo wa kuweza kung'amua uhitaji wa waombaji mikopo, Bodi ililazimika kutoa mikopo kwa asilimia 100 kwa waombaji wote katika mwaka wa masomo wa 2005/2006.

Bodi ilianza kutumia chombo cha kutambua uhitaji wa mwanafunzi (Means testing) katika mwaka wa masomo wa 2006/2007 ambapo kutokana na chombo hicho kuwarundika waombaji wengi katika kundi la kustahili kukopeshwa kwa asilimia 40, Serikali iliagiza kwamba ili kuwapa waombaji unafuu, mikopo ilitolewe kwa asilimia 60 na wanafunzi walitakiwa kuchangia asilimia 40.

Katika mwaka wa masomo wa 2007/08, Bodi iliboresha chombo hicho na kukifanyia majaribio katika shule 53 za Sekondari za bara na visiwani kabla ya kuanza kukitumia na kubainisha kuwa sasa kina uwezo mkubwa wa kung'amua kwa usahihi, uwezo wa waombaji katika uchangiaji, ambapo sasa mikopo inatolewa kwa viwango tofauti kati ya **A(100%), B(80%), C(60%), D(40%), E(20%), na F(0%)** ambapo wanafunzi huchangia asilimia inayobaki.

3.0 MAMBO YANAYOZINGATIWA KATIKA KUNG'AMUA UWEZO WA UCHANGIAJI WA WAOMBAJI MIKOPO

Zoezi la kubaini uwezo wa kiuchumi wa mwombaji hufanywa kwa kutumia taarifa ambazo mwombaji amezitoa katika fomu ya maombi ya mkopo. Taarifa hizo huchukuliwa na kuingizwa katika mfumo wa kompyuta ambao hufanya uchambuzi na kupanga madaraja ya uchangiaji kama yalivyoonyeshwa hapo juu.

Mambo yanayozingatiwa katika ubainishaji wa uwezo wa kiuchumi wa Mwanafunzi na wazazi/walezi wake ni:-

- Historia ya elimu ya mwombaji
- Kiwango cha elimu ya wazazi/walezi
- Shughuli za kiuchumi za mwombaji na wazazi/walezi
- Mali za Mwombaji na wazazi/walezi na Mahali zilipo
- Hadhi ya maisha ya mwombaji na ya wazazi/Walezi wake Kijamii
- Hali ya kijamii ya Mwombaji (Uyatima na Ulemavu)

4.0 MATOKEO YA UNG'AMUZI WA UHITAJI WA MIKOPO (MEANS TESTING RESULTS) KWA MWAKA 2007/2008

Matokeo ya mchanganuo wa uhitaji wa mikopo kwa waombaji wote katika mwaka wa masomo wa 2007/2008 ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini katika Jedwali Na. **1(a)** na **1 (b).**

Jedwali na 1(a): Matokeo ya Mchanganuo wa Uhitaji wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Mwaka wa I 2007/2008

	Asilimia Ya Mkopo unaotolewa	Asilimia ya Kuchangia	Idadi ya wanafunzi	Asilimia yao katika daraja
Kundi A	100	0	2,568	13.59
Kundi B	80	20	10,952	57.92
Kundi C	60	40	4,705	24.88
Kundi D	40	60	647	3.42
Kundi E	20	80	36	0.19
Kundi F	0	100	0	
JUMLA			**18,908**	

Jedwali na 1(b): Matokeo ya Mchanganuo wa Uhitaji wa Mikopo kwa Wanafunzi Wanaoendelea na masomo mwaka 2007/2008

	Asilimia Ya Mikopo unaotolewa	Asilimia ya Kuchangia	Idadi ya wanafunzi	Asilimia yao katika daraja
Kundi A	100	0	19,868	54.03
Kundi B	80	20	8,368	22.75
Kundi C	60	40	8,230	22.38
Kundi D	40	60	280	0.76
Kundi E	20	80	31	0.08
Kundi F	0	100	0	
JUMLA			**36,777**	

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa waombaji wengi wa mikopo wa mwaka wa kwanza (2007/2008) wanaangukia kwenye kundi **B (57.92%)** ambao walikopeshwa **asilimia 80** na kwa wale wanaoendelea na masomo wengi wao **(54.03%)** wanaangukia katika **kundi "A"** ambao walikopeshwa **asilimia 100** ya gharama za Ada, mafunzo kwa vitendo na Mahitaji Maalumu ya Kitivo.

Hivyo, zaidi ya **asilimia 71** ya Wanafunzi wa mwaka wa kwanza (2007/2008) walikopeshwa aidha **asilimia 80** au **asilimia 100** ya mahitaji yao. Aidha, kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo, idadi kubwa **(76.78%)** walikopeshwa aidha **asilimia 80** au **asilimia 100** ya mahitaji yao.

Hii ina maana kuwa kwa ujumla idadi kubwa (74%) ya wanafunzi wote wa vyuo vya elimu ya juu walipatiwa mikopo ya zaidi ya **asilimia 80** ya mahitaji yao na wao kuchangia aidha **asilimia 20** au **asilimia 0**.

Aidha takwimu zinaonyesha kuwa wanafunzi wachache sana wanaangukia katika makundi ya **D, E na F** (wanaochangia asilimia 60, 80 na 100) ambapo ni kiasi cha **asilimia 3.61** kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na **asilimia 0.84** kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo.

Taswira inayoonyeshwa na takwimu hizi ni kuwa wanafunzi walio wengi wanapata mikopo kwa asilimia kubwa kinyume na madai ya wanafunzi kuwa wengi wanapata mikopo kwa asilimia ndogo. Hali hii inasadifiana na hoja za wanafunzi kuwa Watanzania walio wengi hawana uwezo mkubwa kiuchumi na hivyo wanahitaji mikopo kwa asilimia kubwa na hicho ndicho kinachotolewa na Bodi ya Mikopo hadi sasa.

5.0 HITIMISHO

5.1 Hoja zinazotolewa na wanafunzi kuwa zoezi la kubaini uhitaji wa wanafunzi halifanyiki na badala yake Bodi inafuata namba za usajili au alfabeti za majina, ni za uongo mtupu. Serikali za wanafunzi waliombwa kuleta ushahidi kuhusu hoja hiyo lakini wameshindwa kuthibitisha dai hilo. Badala yake wameleta ripoti ya kamati iliyoundwa na Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam (DARUSO) ambayo haitoi ushahidi wowote wa "Means Testing grades" kuendana na namba za usajili (Registration Numbers) wala alfabeti.

Ukweli ni kwamba, wanafunzi wana agenda yao ya siri ambayo ni kutotaka suala la uchangiaji kabisa na badala yake wanataka aidha wapewe ruzuku (grants) au mikopo kwa asilimia 100. Agenda hiyo

ya siri wanajaribu kuipitishia kwenye mgongo wa "Means Testing" inayofanywa na Bodi wakidai kuwa ina hitilafu wakati wakijua fika kwamba kwa kiasi kikubwa taarifa wanazojaza kwenye fomu za maombi ndizo zenye hitilafu.

5.2 Zoezi la kubaini uwezo wa kiuchumi wa waombaji wa mikopo hufanywa kwa umakini mkubwa na mikopo yote hutolewa kwa kuzingatia makundi yaliyopangwa. Ili kulifanya zoezi hili lifanikiwe, waombaji wanapaswa kuzingatia umuhimu wa kujaza fomu za maombi ya mikopo kwa usahihi bila kutoa taarifa za uongo. Kama watatoa taarifa za kweli zikiwemo zinazo wahusu wao na wazazi/walezi wao pamoja na kutaja majina sahihi, matokeo ya "Means testing" yataboreka na kutoa taswira sahihi zaidi ya uhitaji wao.

5.3 Utoaji wa mikopo unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo Na 9 ya mwaka 2004 pamoja na kanuni na miongozo ya utoaji mikopo na vigezo vilivyowekwa. Sheria hiyo inaweka bayana wanafunzi wanaostahili kupata mikopo kuwa sharti wawe ni wahitaji (needy applicants). Hivyo, utaratibu wa kuwabaini wahitaji wa mikopo unatokana na sheria.

5.4 "Means Testing" ndiyo njia pekee iliyopo kwa sasa ya kuwatambua wanafunzi wahitaji na kuainisha viwango vya mikopo wanavyostahili kupata kwani uhitaji wa kila mwombaji mkopo hutofautiana na mwingine. Kwa vile "Means Testing" ni utaratibu wa kisera na kisheria, utaratibu huu utaendelea kutumika mpaka Bodi iamriwe vinginevyo.

IMETOLEWA NA:

MKURUGENZI MTENDAJI
BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU